TANGAZO LA SERIKALI NA. 669 la tarehe 15/9/2023

SHERIA YA PETROLI,
(SURA YA 392)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 29(2)(b))*

AMRI YA GHARAMA ZA UENDESHAJI WA KITUO CHA GESI ASILIA ILIYOSHINDILIWA ZA KITUO KIKUU, KITUO KIDOGO, KITUO CHA KUJAZIA GESI KATIKA MAGARI KILICHOUNGANISHWA KATIKA MTANDAO WA KUSAMBAZIA GESI ASILIA, KITUO CHA KUJAZIA GESI KATIKA MAGARI AMBACHO HAKIJAUNGANISHWA KATIKA MTANDAO WA KUSAMBAZIA GESI ASILIA NA BEI KIKOMO KWA WATUMIAJI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Gharama za Uendeshaji wa Kituo cha Gesi Asilia Iliyoshindiliwa za Kituo Kikuu, Kituo Kidogo, Kituo cha Kujazia Gesi Katika Magari Kilichounganishwa Katika Mtandao wa Gesi Asilia, Kituo cha Kujazia Gesi Katika Magari ambacho Hakijaunganishwa katika Mtandao wa Kusambazia Gesi Asilia na Bei Kikomo kwa Watumiaji ya Mwaka 2023.

Tafsiri

2. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"bei ya mtumiaji wa mwisho" maana yake ni bei kikomo ambayo huzingatia gharama zote katika mnyororo wa thamani na kuidhinishwa na Mamlaka ambayo hutozwa na mwenye kituo kwa wateja wake;

"gesi asilia iliyoshindiliwa" maana yake ni gesi asilia katika mfumo wa mchanganyiko wa gesi na mivuke ya hidrokaboni, inayojumuisha hasa

methane (CH4) ambayo imeshindiliwa;

"gharama" maana yake ni gharama zote za lazima za ujenzi, uendeshaji, ukarabati na faida kwa aina maalum ya kituo cha gesi asilia iliyoshindiliwa;

"kituo kikuu" maana yake ni kituo kilichounganishwa katika bomba la kusambazia gesi asilia na huwa na vifaa kama kompresa, kifaa cha kusafishia gesi asilia, hifadhi ya gesi iliyoshindiliwa, mita, vifaa vya utambuzi wa gesi iliyovuja, vifaa vya kuzimia moto, vifaa vya kujazia gesi katika hifadhi ya gesi inayohamishika, na ikiwa kutakuwepo na mashine za kujazia gesi, kinaweza kujaza gesi katika magari yanayotumia gesi iliyoshindiliwa;

"kituo kidogo" maana yake ni kituo ambacho hakijaunganishwa katika bomba la kusambazia gesi asilia na huwa na vifaa kama, hifadhi ya gesi inayohamishika, hifadhi ya gesi isiyohamishika, vifaa vya utambuzi wa gesi iliyovuja na vifaa vya kuzimia moto. Kituo hiki hujaza gesi iliyoshindiliwa katika viwanda;

"kituo kilichounganishwa katika bomba la gesi asilia" maana yake ni kituo ambacho kimeunganishwa katika bomba la kusambazia gesi asilia na huwa na vifaa kama kompresa, hifadhi ya gesi isiyohamishika, mashine za kujazia gesi, vifaa vya utambuzi wa gesi iliyovuja na vifaa vya kuzimia moto;

"kituo ambacho hakijaunganishwa katika bomba la gesi asilia" maana yake ni kituo ambacho hakijaunganishwa katika bomba la kusambazia gesi asilia na huwa na vifaa kama kompresa ndogo, hifadhi ya gesi inayohamishika, hifadhi ya gesi iliyoshindiliwa, mashine za kujazia gesi, vifaa vya utambuzi wa gesi iliyovuja na vifaa vya kuzimia moto; na

Sura ya 414

"Mamlaka" au "EWURA" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

Gharama za uendeshaji na bei kikomo kwa mtumiaji

3. Gharama za uendeshaji wa kituo cha gesi asilia iliyoshindiliwa za kituo kikuu, kituo kidogo, kituo cha kujazia gesi katika magari kilichounganishwa katika mtandao wa gesi asilia, kituo cha kujazia gesi katika magari ambacho hakijaunganishwa katika mtandao wa gesi asilia na bei kikomo kwa watumiaji zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na la Pili la Amri hii.

Mapitio ya bei kikomo kwa mtumiaji wa mwisho

4. Bei kikomo ya mtumiaji wa mwisho wa gesi asilia iliyoshindiliwa inaweza kurekebishwa kuzingatia mabadiliko ya bei ya gesi asilia ya kisima na tozo za miundombinu iliyopo ya gesi asilia au pale Mamlaka itakapoona inafaa.

Masharti ya gizo

5. Gharama za uendeshaji wa vituo vya kushindilia gesi asilia na bei kikomo za mtumiaji zilizoidhinishwa zina ambatana na masharti yafuatayo:

(a) mwenye leseni, atawasilisha kwa EWURA gharama halisi za mradi ndani ya miezi sita baada ya tarehe ya kuanza utekelezaji wa mradi;
(b) wote wenye leseni ya vituo vya gesi asilia iliyoshindiliwa, kila ifikapo tarehe 30 Aprili kila mwaka, watawasilisha EWURA taarifa za gharama za uendeshaji na matengenezo ikijumuisha kodi na tozo zinazolipwa kwa taasisi mbalimbali za Serikali, na taarifa hizo zinapaswa kuwasilishwa kwenye *excel* ambayo

inabadilishika pamoja na viambatisho kama vile risiti;

(c) mwenye leseni ya kituo cha gesi asilia iliyoshindiliwa, kila mwezi atawasilisha EWURA kiasi cha gesi asilia alichonunua na kuuza kupitia mfumo wa kitaifa wa taarifa za petroli na gesi na kupitia barua pepe maalum za EWURA;

(d) miezi sita kutoka tarehe ya kutangazwa kwa Amri hii wamiliki wote wapya wa leseni za vituo vya gesi asilia iliyoshindiliwa wanatakiwa kuwasilisha EWURA rasimu ya mkataba wa huduma kwa wateja unaohusiana na huduma za gesi asilia iliyoshindiliwa kwa mapitio na kuidhinishwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Petroli (Gesi Asilia) wa Mwaka 2019; na

(e) wenye leseni za vituo vikuu na vile vilivyounganishwa katika mtandao wa gesi asilia, watawasilisha EWURA makubaliano ya awali ya mauzo ya gesi asilia kabla ya kusainiwa wakati wa kuomba kibali cha awali cha ujenzi kwa ajili ya mapitio.

______________

**JEDWALI LA KWANZA**

______________

*(Limetengenezwa chini ya Amri ya 4)*

GHARAMA ZILIZOIDHINISHWA ZA UENDESHAJI ZA VITUO VYA GESI ASILIA ILIYOSHINDILIWA

| Aina ya Kituo | Shilingi/Kilo |
|---|---|
| **Kituo Kikuu** | 83 |
| **kituo kilichounganishwa katika bomba la gesi asilia** | 634 |
| **kituo cha nje ya mtandao wa bomba la gesi asilia** | 669 |
| **Kituo Kidogo kwa ajii ya wateja wa viwanda** | 90 |

**JEDWALI LA PILI**

(*Limetengenezwa chini ya amri ya 4)*

BEI KIKOMO ZILIZOIDHINISHWA ZA GESI ASILIA ILIYOSHINDILIWA KWA BAADHI YA MIKOA/WILAYA

| Mkoa / Wilaya | Kituo kilichounganishwa / kituo cha nje ya mtandao wa bomba la gesi asilia | Kituo Kidogo kwa Matumizi ya Viwandani |
|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | 1,548 | 967 |
| **Kibaha** | 1,621 | 1,040 |
| **Mlandizi** | 1,668 | 1,086 |
| **Chalinze** | 1,775 | 1,194 |
| **Bagamoyo** | 1,692 | 1,111 |
| **Mkuranga** | 1,548 | 967 |

| | | |
|---|---|---|
| **Kisarawe** | 1,611 | 1,030 |
| **Morogoro** | 1,950 | 1,368 |
| **Lindi** | 1,548 | 967 |
| **Mtwara** | 1,548 | 967 |

Dodoma, JAMES A. MWAINYEKULE
……………….., 2023 *Mkurugenzi Mkuu*